Name ……………………………………………………………………………. Adm No…………. Class………. No……….Sign…………….

NYABURURU GIRLS' NATIONAL SCHOOL

OUR LADY OF LOURDES

**KISWAHILI KIDATO CHA PILI**
**MJARABU WA KWANZA**
**MUHULA WA TATU 2017**
**MUDA: MASAA MAWILI**

| | |
|---|---|
| ***Tarehe*** | |
| ***Msimamizi*** | |
| ***Kurejeshwa*** | |
| ***Kudurusu*** | |

**Maagizo**

- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| FASIHI SIMULIZI | 15 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Tarakilishi ama kompyuta ni kati ya teknolojia mpya ambayo inatumiwa siku hizi karibu kila mahali kwa mfano katika makampuni makubwa makubwa, benki, masoko makubwa makubwa, viwandani, viwanja vya ndege, meli, idara za serikali, vyuo, shuleni, na kadhalika. Katika shule za upili, takakilishi ni somo ambalo linashughulikiwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na hutahiniwa katika mtihani wa kidato cha nne: KCSE.

Tarakilishi imegawanyika katika sehemu mbili muhimu. **Programu** mfumo na maunzi. Maunzi ni neno jumlishi ambalo hutumika kwa kurejelea vifaa vyote vya kompyuta kwa mfano kichapishi, kishalekezi, skrini, **kipanya** na mashine chapishi. Programu mfumo ni neno jumlishi ambalo hurejelea programu zote zinazoweza kutumika katika kompyuta.

Vifaa vinavyotumika katika kompyuta ni vingi. Skrini katika kompyuta hutumika kwa kuonyesha **data** ambayo inashughulikiwa, nacho kichapishi hutumika katika kuvugulia data hiyo kwa kompyuta. **Kishalekezi** ni kifaa ambacho huwaka kikizimika kwa skrini, nacho huashiria pahali ambapo data **inayovuguliwa** itaingia. Pahali pa kishalekezi panaweza kubadilishwa kwa kutumia kipanya. Kipanya ni kidude kilicho na mkia mithili ya panya. Baada ya kazi kukamilika na data kuwa habari, mashine chapishi huichapisha **habari** hiyo kwa karatasi ili isomwe na watu wengi iwezekanavyo, pahali pengi na pahali popote.

Tarakishi ina sifa nyingi muhimu ambazo tutaziainisha. Chombo hiki kina uwezo wa kufanya hesabu na kazi nyingine nyingi kwa kasi sana. Sifa nyingine ni kwamba tarakilishi **huhifadhi** ujumbe mwingi sana kwa matumizi ya baadaye. Maelekezo huchukuliwa na kuwekwa kwa ajili ya kufuatwa na chombo hiki. Mfululizo wa maelekezo haya ndio huongeza kompyuta katika kutekeleza wajjibu wake na huitwa programu ambayo huandikwa kwa lugha ya kikompyuta. Kompyuta hufuata maelekezo haya kwa kuamshwa na binadamu. Sheria hizi huwa sahili na kompyuta ina uwezo wa kuzitumia ili kufikia uamuzi wa jinsi ya kutenda.

Kuwasiliana na mifumo mingine ya kompyuta ni muhimu sana na kompyuta ina uwezo wa kufanya hivyo. Kompyuta huingizwa data ambayto huchakatwa ili kulete maana, na uzao wa **kuchakatwa** huku ndio huitwa habari. Programu huiwezesha kompyuta kuchakata data na kuifanya iwe habari kwa mfano, inaweza kuongeza nambari mbili au zaidi na kukupa jibu.

Katika kompyuta habari inaweza kuhifadhiwa katika diski ngumu au diski tepetevu. Diski ngumu ni nafasi inayopatikana katika kompyuta yenyewe na inaweza kuhifadhi maktaba nzima. Diski tepetevu ni ile nafasi ambamo disketi huwekwa ili habari inayochakatwa ihifadhiwe kwa disketi. Disketi ni kifaa kidogo mithili ya kaseti. Nafasi hizi za kompyuta zimegawanywa katika viendesha diski kwa mfano ukitaka kuhifadhi habari yako kwa diski ngumu, utatumia **kiendesha diski A**: ilhali ukitaka kuhifadhi kazi yako katika diski tepetevu, utatumia kiendesha diski C.

Kwa muhtasari, tunaweza kusema kwamba kompyuta ni kifaa au chombo ambacho hufanya kazi kwa kuongozwa na programu iliyohifadhiwa. Kompyuta hujiendesha yenyewe kwa kukubali na kuchakata data ili iwe habari.

**Maswali**

(a) Toa neno lingine lenye maana sawa na tarakilishi. (al.1)

(i)

(b) Toa mifano mitatu ya pahali ambapo tarakilishi hutumika. (al.3)

(i)

(ii)

(iii)

(c) Ni sehemu gani mbili ambazo tarakilishi imegawanyika. Toa ufafanuzi wa sehemu hizi. (al.4)

(i) –

(ii) –

Ufafanuzi

(i) –

(ii) –

(d) Eleza kazi ya vifaa vifuatavyo:- (al.2)

(i) Kipanya –

(ii) Kichapishi –

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika makala haya. (al.5)

(i) Data –

(ii) Inayovuguliwa –

(iii) Huhifadhi –

(iv) Kuchakata –

(v) Kiendesha diski –

## 2. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Eleza maana ya mofimu huru na uitolee mfano. (al.2)

(i)

(ii)

(b) Tunga sentensi moja inayotumia neno kupika kama nomino. (al.2)

(c) Toa mifano miwili ya nomino za wingi na mingine miwili ya nomino za dhahania. (al.4)

(i)

(ii)

(d) Tumia kivumishi nadhifu kutungia sentensi katika ngeli ya A-WA. (al.2)

(e) Andika wingi wa sentensi: (al.2)

Mfanyibiashara yeyote atakayepatikana na pembe za ndovu atafungwa.

(f) Andika sentensi ifuatayo ukitumia ‘O’ rejeshi. (al.2)

Mto ambao umefurika umevunja kingo zake.

(g) Onyesha viambishi awali, tamati na mzizi katika alisahaulika. (al.4)

(h) Tambulisha vitenzi visaidizi katika sentensi hizi. (al.2)

(i) Tungali tunaandika

(ii) Hajaenda kusoma

(i) Onyesha viwakilishi katika sentensi hizi. (al.2)

(i) Mtoto anacheza uwanjani

(ii) Manukato haya yananukia

(j) Tunga sentensi mbili ukitumia:

(i) Vivumishi vya idadi kamili (al.1)

(ii) Vivumishi vya jumla ya idadi (al.1)

(k) Tunga sentensi ukitumia viashiria visisitizi vifuatavyo. (al.2)

(i) Vivyo hivyo

(ii) Uu huu

(l) Tumia maneno haya katika sentensi. (al.2)

(i) Wengine

(ii) Kwingineko

(m) Tunga sentensi tatu tofauti ambapo. (al.3)

(i) Vielezi vinafafanua vitenzi

(ii) Vielezi vinafafanua vivumishi

(iii) Vielezi vinafafanua vielezi vingine

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (al.4)

Watoto walighani shairi lote

(o) Andika kwa udogo: (al.2)

Alipopiga ngoma ile wote waliamka

(p) Unda nomino kutoka na nomino. (al.2)

(i) Hodari

(ii) Mpenzi

(q) Tunga sentensi ukitumia alama hii ya uakifishi. (:) (al.1)

## 3. <u>FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)</u>

(a) Taja vipera vinne vya semi. (al.4)

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(b) Taja sifa nne za malumbano ya utani. (al.4)

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

(vi)

(c) Taja vipera vitano vya mazungumzo. (al.5)

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

(d) (i) Ngano ni aina gani ya hadithi? (al.1)

(ii) Na je tarihi? (al.1)

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Eleza ni mambo gani husababisha tofauti katika sajili za lugha.